# MSIPOWASAMEHE WATU MAKOSA YAO…

## *Baba Yenu Hatawasamehe Ninyi Makosa Yenu*

# ?

**Shemeji Melayeki**

**MSIPOWASAMEHE WATU MAKOSA YAO…**

**© 2025**

**Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565

+255 763 965 297

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: *@melayeki*
Facebook: *Apostle Shemeji Melayeki*

**ISBN - 978-9912-9884-8-4**

Kimepigwa Chapa Na: **KLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA**

**+255 658 288 054**

**+255 687 699 862**

# YALIYOMO

SHUKRANI....................iii
SURA YA 1.................... 1
*MAMBO YA MSINGI*.................... 1
SURA YA 2.................... 8
*KUHUSU MSAMAHA WA DHAMBI*.................... 8
SURA YA 3.................... 24
*KWA HIYO YESU ALIMAANISHA NINI?*.................... 24

# SHUKRANI

Nilikwama katika namna yangu ya kufasiri Biblia hadi nilipopata mafundisho ya Mchungaji Chris Onayinka. Namna yangu ya kufasiri Biblia ilibadilika na kupokea mwanga mpya wa kuyaona maandiko matakatifu. Mafundisho na maandishi yangu yameathiriwa na namna yake yenye faida kubwa katika usahihi wa kuyasoma na kuyaelewa maandiko. Ninashukuru sana kwamba huduma yake inaendelea kunijenga na hatimaye huduma yetu.

Kwa familia yangu, mara nyingi nimekuwa macho usiku wakati wamelala, kwa utulivu mkubwa walionipa. Mke wangu Neema amekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha ninafanikisha uandaaji wa kitabu hiki.

Kwa timu ya watu waliojitolea kujifunza kupitia kwangu kwenye huduma ya Global Family Gatherings; wachungaji wetu na maaskofu, wamekuwa sababu ya kunifanya nijitume zaidi.

Kwa wadau wanaofanya huduma pamoja na mimi kwa njia ya sadaka zao ili kuhakikisha kazi hii haikwami, wamekuwa waaminifu kwa rasilimali zao ili kweli hii ienee zaidi.

# SURA YA 1

## *MAMBO YA MSINGI*

Hekima ya maandiko ni msaada wetu kuhusiana na msamaha wa dhambi. **2 Timotheo 3:15-16** *[15] na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. [16] Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki;*

Neno "**kukuhekimisha**" kwenye lugha ya asili ya Biblia linamaanisha *kuwa na akili na ustadi; ili kubuni mambo kwa ustadi*.

Neno "**umeyajua**" kwenye lugha ya asili ya Biblia linamaanisha *kuona kwa macho na kuthamini*. Kwa hiyo, Paulo katika andiko lililo juu anadokeza kwamba Timotheo alikuwa na uwezo wa kutumia na kuthamini

maandiko kwa njia ifaayo. Neno hilohilo lilitumiwa tena na Paulo katika barua yake ya pili.

Paulo alitumia maneno "**Kila andiko**" katika mstari wa 16 na "**maandiko matakatifu**" katika mstari wa 15. Ona kwamba matumizi ya neno hilo katika Mstari wa 16 ni umoja (andiko) huku mstari wa 15 ukitumia maana ya wingi (maandiko).

Katika mstari wa 15, neno "**takatifu**" awali linamaanisha iliyotengwa au ya pekee; ambayo imetengwa kwa kusudi au matumizi maalumu.

Kwa hivyo, Paulo alipoandika "umejua maandiko matakatifu", bila shaka alikuwa akimaanisha Timotheo amesoma kitabu. Hiyo ina maana ujuzi wa Timotheo uliwasilishwa kwa kusoma. Neno "umeyajua" katika andiko hilo linamaanisha Timotheo alikuwa anayafahamu maandiko. Hilo linadokeza kwamba alikuwa amesoma habari hiyo vizuri na kwa kina na kuweza kusema kutoka kwenye maandiko hayo, kunukuu kutoka kwayo na kuelewa mawazo ambayo yalipitishwa ndani ya hayo maandiko.

Neno maandiko katika mstari wa 15 awali lilirejelewa pia kwa vitu vinavyochorwa na pia huelezea kitendo chenyewe cha kuandika. (2 Wakorintho 3:3 (iliyoandikwa), Wagalatia 6:11 (nimewaandikia).

Neno "**andiko**" katika mstari wa 16 hapo awali lilimaanisha mkusanyiko wa vitabu vya Agano la Kale (Mwanzo mpaka Malaki).

Kwa hiyo Paulo katika mstari wa 16 anasema MAANDIKO YOTE yametolewa kwa pumzi ya Mungu.

Kwa hiyo hii inaashiria kwamba Paulo katika 2 Timotheo 3:16 alikuwa akimaanisha maudhui ya maandiko matakatifu ni kushughulika na mambo aliyoyataja hapo.

Kifungu cha maneno ***"lenye pumzi ya Mungu"*** kilimaanisha kuhimiza au kuhamasisha mtu au kitu kingine au kwa lugha rahisi kuvuvia.

Hivyo, Paulo alikuwa akisema hapa kwamba uandikaji wa maandishi hayo yalivuviwa na Roho ya Mungu. Mungu aliwavuvia wale walioiandika.

Kwa hiyo maandiko matakatifu yanafaa ***kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.***

Anaongezea kwa kusema **2 Timotheo 3:17** *[17] ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*

Kwa hiyo ni kwa ajili ya watu wa Mungu au waamini au wenye haki. Inaelekeza namna atakavyoenenda.

Angalia tena Tafsiri ya Kiswahili SUV inatumia "…kukuhekimisha hata upate wokovu" ila ilitakiwa kusomeka hivi "…. kukuhekimisha **katika wokovu**".

Neno *upate* ukisoma King James Version ni *unto* ambapo tafsiri mojawapo ni *katika.* Hii ni kwa sababu Timotheo tayari alikuwa ameokoka na maandiko kwake yana lengo la kumpa maelekezo au hekima ya kuenenda katika wokovu. Hivyo tungesema *umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha KATIKA wokovu.* Hekimisha imetokana na neno lenye mzizi wa hekima (**sophizo** - *to make wise, teach, to have understanding*), akimaanisha kuwa maandiko yanaweza kukuhekimisha jinsi ya **kuenenda katika wokovu**. Hivyo, lengo la Maandiko Matakatifu ni kuhekimisha katika wokovu.

**2 Timotheo 3:15** *[15] na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu.*

Neno "**kujua**", katika kigiriki ni '**eido**' (to perceive with eyes) yaani, mtazamo unaokuwa nao unapofanya jambo fulani, katika muktadha huu ni ule mtazamo anaokuwa nao mtu anaposoma maandiko matakatifu. Maandiko matakatifu kwa muktadha huu ni Mwanzo mpaka Malaki kwani hivyo ndivyo vitabu vilivosomwa na kanisa la kwanza.

Kwa hiyo utakatifu maana yake ni kile kilichotengwa kwa ajili ya kusudi maalumu. Hivyo, maandiko matakatifu yamechaguliwa kwa kusudi/lengo maalumu na hapa **2Timotheo 3:15** Paulo anasema kuwa kusudi la maandiko matakatifu ni **kujifunzia na kufundishia.**

Kuonya –*Reproof* '**Elegchos**' *(a proof by which a thing is proved or tested)* yaani kukupa Ushahidi mwingi.

Kuwaongoza –*Correction kwa Kiyunani ni* '**Epanorthosis'***(Restoration to an upright or right state, correction, improvement of life or character)* kurekebisha mtindo wa maisha na mwenendo wa watu.

Kuadibishwa = *Instructions*= **'Paideia'**= *(The whole training and education of children)* = Kuelezea mafundisho kwa mtoto.

Hii ndio sababu mkristo hahitaji na hapaswi kuongozwa na Saikolojia yeyote, kwa sababu Neno la Mungu lina maelekezo ya kutosha kuhusu mwenendo wake. Hivyo hakuna jambo ambalo mkristo atashindwa kufanya kwa sababu mtazamo wake unaongozwa na Neno. Hakuna kitu kama, "…Ndio hivyo nilivyo". Mwamini hayuko chini ya cho chote, bali vyote vipo chini yake anaweza kuelekeza matamanio yake sawa sawa na maandiko matakatifu.
**2 Timotheo 3:17***[17]* "*ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"*.
Neno amekamilishwa limetafsiriwa kutoka kwenye neno *'thoroughly furnished'* likitokana na neno **exartizo** *(To complete or finish perfect/accomplish) that is to equip fully* yaani ametayarishwa/amewezeshwa kwa Habari ya mwenendo kama mkristo na kwa Habari ya Injili.
*Neno 'Kamili'* limetokana na neno '**Artios'** ***(****Perfect***)** *fitted, complete* yaani Mwenendo wa Mkristo na Injili.

**Waefeso 4:11-12** *[11] Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu. [12]kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.*

"…Kukamilisha watakatifu" ndio kusema kuwawezesha (capacity building) kufanya vizuri kazi ya huduma, mwili wa Kristo ujengwe na kazi ya huduma itendeke. Lengo ni kuwawezesha waweze **kufanya huduma, yaani azae watu watakaofanya kama yeye** kwasababu kila Mwamini ni '**MHUDUMU**' wa injili na anakuwa katika mwenendo na utendaji wa huduma.

***"...ili tusiwe tena watoto wachanga…"***

Mhudumu huyu anafundishwa lililokuwa sahihi. Kama watu wa taasisi za fedha, jambo muhimu ni kuelekezwa juu ya noti halisi (*originalnote*) ili aweze kuijua vizuri na wala hafundishwi kuhusu noti feki, kwa sababu, feki ni nyingi sana, ila "**HALISI**" inabaki kuwa na sifa zile zile nyakati zote.

Tunapoendelea katika somo hili, ni muhimu kuelewa kwamba kanuni ya msingi ya ufasiri sahihi wa Biblia ni kwamba kifungu cha Maandiko hakiwezi kumaanisha leo kile ambacho hakijawahi kumaanisha wakati kilipoandikwa. Kwa hiyo, hitaji la kutafsiri kwa bidii na kwa usahihi Maandiko, vinginevyo kiini hasa kilichofanya Biblia hiyo kuandikwa kingeshindwa na kupotea kabisa. Kwa hiyo, umuhimu wa kufasiri Maandiko kwa bidii ni lazima kusisitizwa sana.

Uangalifu lazima uzingatiwe ili kufasiri muktadha, maudhui, sarufi, msamiati, ukweli wa kihistoria, nyakati na tamathali za usemi kama zilivyotumiwa na mwandishi.

Hivyo, katika kufasiri Biblia, lazima uangalie kwa makini matumizi ya maneno, kwa sababu kama ilivyosemwa hapo awali "maandiko hayawezi kamwe kumaanisha leo, yale ambayo mwandishi hakumaanisha wakati anaandika." Hili linatupa ulazima wa kuwa makini na kuzingatia matumizi ya maneno kama vile muundo wa kisarufi, uchanganuzi wa muktadha, matumizi ya kihistoria ya maneno, na jinsi maneno hayo yanavyotumiwa katika muktadha wa kitabu na vitabu vingine na waandishi wengine wa Biblia.

Sasa, tuanze kuangalia juu ya MSAMAHA WA DHAMBI na maneno ya Bwana wetu Yesu Kristo.

# SURA YA 2

## *KUHUSU MSAMAHA WA DHAMBI*

Malaika alimtokea Yusufu na kumwambia…**Mathayo 1:20-21** *[20] Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. [21] Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake YESU, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*

Angalia maneno ya malaika.. *ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao* ametaja moja kwa moja kazi ya Yesu au lengo la kuja katika mwili, kuwaokoa watu kwenye hatari mahususi ambayo ni dhambi zao.

Tazama **Luka 24:44-49** *[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. [45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate*

*kuelewa na **maandiko**. [46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; [47]na kwamba mataifa yote WATAHUBIRIWA kwa jina lake habari ya toba na **ondoleo la dhambi**, kuanza tangu Yerusalemu. [48] Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. [49] Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.*

Ujumbe wa Injili unaweza kuelezwa kama AHADI KWENYE VITABU VYA AGANO LA KALE AMBAYO KRISTO ATAKUJA NA KUITIMIZA KWA KUPATA MATESO, KUFA NA KUFUFUKA KWAKE NA KWA SABABU HIYO TOBA NA MSAMAHA WA DHAMBI **KUHUBIRIWA.** Hii ndio sababu Injili inahubiriwa.

Angalia hapa pia, *watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na **ondoleo la dhambi.*** Je, toba ni nini? Toba ni neno la Kigiriki **metanoia** lenye maana badiliko la fikra na mwelekeo na hii hutokea zaidi baada ya kusikia ujumbe. Hebu tutazame namna neno hili **metanoia** lilivyotumika katika Biblia. Mzizi wa neno **metanoia** ni **metanoeō** lenye maana ya *kufikiri tofauti baadae.*

**Marko 1:15** *[15] akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.*

*…tubuni na kuiamini Injili.* Kubadili fikra kwa kuiamini Injili.

**Mathayo 12:41** *[41] Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.*

…kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; *walibadilika katika fikra zao, walisadiki ujumbe wake.* Kwa hiyo KUTUBU NI KUPOKEA UJUMBE.

Neno **kutubu** limekuwa likitumika kwa umaarufu katika jamii yetu kama KUOMBA MSAMAHA BAADA YA KUFANYA KOSA. Maana ya Biblia ya kutubu sio hii kabisa. Kutubu sio matokeo ya kukosea kwa mtu bali ujumbe aliosikia (Injili).

Baada ya mahubiri marefu ya Petro kwenye Matendo 2, anawaagiza wasikilizaji wake kutubu. **Matendo 2:37-38** *[37]Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu? [38]Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

Wakamwambia Petro, tutendeje ndugu zetu? Tubuni mpate ondoleo la dhambi zenu.

Hapa tena baada ya kuhubiri; **Matendo 3:19** *[19] Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;*

Tubuni ili dhambi zenu zifutwe.

**Matendo 5:31** *[31] Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi*.

Awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.

**Matendo 10:43** *[43] Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

**Kila amwaminiye** atapata ondoleo la dhambi.

Hapa Petro ametumia maneno KILA AMWAMINIYE ambapo ni sawa na kusema TUBUNI.

Kwa **muktadha** huu KUTUBU ni kile kinachotokea baada ya mtu kusikia Injili yaani habari za *kufa na kufufuka kwa Yesu*. Matokeo ya badiliko hili la nia ni kupokea MSAMAHA WA DHAMBI. Hii ni kwa imani (kwa kuamini Injili).

Msamaha wa dhambi au ondoleo la dhambi ni neno moja la Kigiriki **APHESIS** ambalo lina mzizi kutoka kwenye neno **APHIEMI…**lenye maana ya (English) -- *release from the bondage or imprisonment, pardon of sins (letting them go as if they had never been commited), remission of the penalty.*[Kiswahili] *kuachiliwa au kuondolewa kifungoni, kusamehe au kuziachilia dhambi kana kwamba hayajawahi kufanyika.* Huu ndio ubora wa dhabihu ya Yesu Kristo. Hivi ndivyo Mungu anafanya kwa mwamini. Dhambi zake zimeondolewa, zimefutwa.

Maneno yote mawili, MSAMAHA WA DHAMBI na ONDOLEO LA DHAMBI yametafsiriwa kutoka kwenye neno hili moja la Kigiriki **APHESIS.**

**Matendo 5:29-31** *[29] Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. [30]Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. [31] Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.*

Anawataka pia watubu (waamini) katika kufa na kufufuka kwake ili wapokee Msamaha wa dhambi.

Nyuma kwenye sura ya 2, Petro alihubiri vivyo hivyo;

**Matendo 2:38** *[38] Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

Tubuni mpate ondoleo la dhambi zenu. Neno la Kigiriki la ondoleo la dhambi na Msamaha wa dhambi ni moja **APHESIS.**

**Matendo 10:42-43** *[42] Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu. [43] Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa* ***jina lake*** *kila* ***amwaminiye*** *atapata* ***ondoleo*** *la dhambi.*

Kwenye nyumba ya Kornelio pia alihubiri habari za kufa

na kufufuka kwake Yesu hivyo kupata*ondoleo la dhambi kwa kila aaminiye.*

Ukweli ni kwamba Kornelio alikuwa na mwenendo mzuri laki hakuwa ameokoka, angalia hapa… **Matendo ya Mitume 10:1-4** *[1] Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, [2] mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima. [3] Akaona katika maono waziwazi, kama saa tisa ya mchana, malaika wa Mungu, akimjia na kumwambia, Kornelio! [4] Akamtazama sana, akaogopa akasema, Kuna nini, Bwana? Akamwambia, Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu.*

Kornelio alikuwa

- *Mtu mtauwa,*
- *Mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote,*
- *Alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi,*
- *Alikuwa anamwomba Mungu daima.*
- *Aliona katika maono waziwazi*

Lakinia Kornelio alikuwa hakuwa ameokoka/ameokolewa.

Angalia, **Matendo ya Mitume 10:5-6** *[5] Sasa basi, peleka watu Yafa, ukamwite Simoni, aitwaye Petro. [6] Yeye ni mgeni wa mtu mmoja, jina lake Simoni,*

*mtengenezaji wa ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani, atakuambia yakupasayo kutenda.*

Malaika anamwambia, Petro *atakuambia yakupasayo kutenda.*

Petro wakati anahubiri habari za Yesu alisema kuhusu Yesu.

Kornelio anatakiwa kutenda nini tena wakati, *Mtu mtauwa, Mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye, Alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na Alikuwa anamwomba Mungu daima pamoja na kuwa alikuwa anaona katika maono waziwazi?*

**Matendo ya Mitume 10:36-43** *[36] Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote), [37] jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianzia Galilaya, baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana; [38] habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye. [39] Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini. [40] Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika, [41]si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka*

*kwake kutoka kwa wafu. [42]Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu. [43] Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

Petro alianza kuelezea habari za mambo yaliyotokea tangu wakati wa ubatizo wa Yohana, na kuwa aliteswa, akafa na akafufuka kisha akasema na kile walichoagizwa kuhubiri kwa habari yake.. akamaliza kwa kusema *Huyo (Yesu) manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa **jina** lake kila **amwaminiye** atapata ondoleo la dhambi.*

Kwa hiyo pamoja na matendo yote mazuri ya Kornelio, kuna jambo moja alilotakiwa kufanya nalo ni ***kuamini ili kupata ondoleo la dhambi.*** Kulingana na Mathayo 1:21, ondoleo la dhambi ni wokovu.

Ndiyo maana Petro alisema kwenye **Matendo ya Mitume 11:13-14** *[13] akatueleza jinsi alivyomwona malaika aliyesimama nyumbani mwake na kumwambia, Tuma watu kwenda Yafa ukamwite Simoni aitwaye Petro, [14]atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote.*

Angalia namna Petro alivyoyaweka maneno ya malaika *atakayekuambia maneno ambayo* ***yatakuokoa****, wewe na nyumba yako yote.*

**Kwa hiyo, Kornelio na nyumba yake yote waliamini mahubiri ya Petro na KUOKOKA.**

Mitume walipomjibu Petro walisema kwenye **Matendo ya Mitume 11:18** *[18]Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*

Angalia namna walirejea kuamini kama toba. Wanasema *Mungu amewajalia hata mataifa nao **toba** liletalo uzima.*

Waliamini au walitubu na kupata uzima au ondoleo la dhambi. Kwa hiyo kwenye matendo ya mitume, toba ilihusishwa na kuamini.

**Matendo 13:37-39** *[37] Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu. [38] Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi; [39] na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.*

**Matendo 26:13-18** *[13] Ee Mfalme, ndipo wakati wa adhuhuri njiani naliona nuru inatoka mbinguni ipitayo mwangaza wa jua, ikinimulikia mimi, na wale waliofuatana nami pande zote. [14] Tukaanguka nchi sote, nikasikia sauti ikisema nami kwa lugha ya kiebrania, Sauli! Sauli! Mbona waniudhi? Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo. [15] Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi. [16] Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayonitajidhihirisha kwako; [17]*

*nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao; [18] uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu;* ***kisha wapate msamaha wa dhambi zao****, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.*

Tazama mkazo wa huduma yake…awafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache **nguvu za giza** na kumwelekea Mungu; **kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi (YESU).**

Mtume Paulo alijua namna ya kuzishinda nguvu za giza (za shetani); ni kwa kuhubiri Injili inayotoa msamaha wa dhambi kwa imani katika Kristo.

Paulo hapa tena,**Matendo 26:22-23** *[22] Basi kwa kuwa nimeupata msaada utokao kwa Mungu nimesimama hata leo hivi nikiwashuhudia wadogo kwa wakubwa,* ***wala sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa; [23] ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru*** *kwa watu wake na kwa watu wa Mataifa.*

Paulo alibaki katika kiini cha ujumbe wa manabii na Musa, habari za kufa na kufufuka kwa Yesu na watu kupokea Nuru (msamaha wa dhambi au kuhesabiwa

haki).

**Waefeso 1:7** *[7] Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

Katika Kristo kwa damu yake tunao masamaha ya dhambi.

**Wakolosai 1:13-14** *[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; [14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;*

Mwamini hasubiri kusamehewa, ANAO msamaha wa dhambi.

Msingi wa msamaha wa dhambi zetu ni dhabihu yake Yesu Kristo au damu yake.

Tazama **1 Yohana 2:1-2** *[1] Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, [2] naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.*

Zingatia matumizi ya nyakati hapa…***tunaye mwombezi…*** Neno ***kipatanisho*** ni neno la Kigiriki **hilasmos** lenye maana ya *sadaka iletayo utakaso*. Yesu ni kipatanisho kwa dhambi za wanadamu, Yeye ndiye sadaka iliyotolewa, hata sasa na milele na anabaki kuwa sadaka ambayo kwayo tumepata UTAKASO. Hakuna

alichosaza.

**Waebrania 8:10-12** *[10] Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli Baada ya siku zile, asema Bwana; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika; Nami nitakuwa Mungu kwao, Nao watakuwa watu wangu. [11] Nao hawatafundishana kila mtu na jirani yake, Na kila mtu na ndugu yake, akisema, Mjue Bwana; Kwa maana wote watanijua, Tangu mdogo wao hata mkubwa wao. [12] Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena.*

Kwenye Agano hili, dhambi na uovu wetu haukumbukwi tena.

Chini ya Sheria, kulikuwa na kumbukumbu la dhambi na sadaka zilizotolewa ni za wanyama. Kwenye Agano jipya, Yesu mwenyewe amejitoa kuwa sadaka kwa ajili ya dhambi zetu.

Tazama **Waebrania 10:3-4** *[3] Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. [4] Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*

Dhabihu za mafahali na mbuzi hazijawahi kumsaidia yeyote, lakini Yesu kwa kujitoa kwake kuwa dhabihu kwa ajili yetu amefanya kazi timilifu.

**Waebrania 10:10** *[10] katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja*

*tu.*

Tazama, ni kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo MARA MOJA TU. Si kila mwaka. Yeye si kama sadaka za Wanyama.

**Waebrania 10:11-12** *[11] Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. [12] Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;*

Yesu hasimami KILA SIKU akifanya ibada, mara moja ALIMALIZA. Ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Kazi yake ameimaliza.

KWA DHABIHU MOJA IDUMUYO HATA MILELE AMEWAKAMILISHA HAO WANAOTAKASWA. **AMETUKAMILISHA.**

Tazama utofauti uliopo kati ya dhabihu ya Yesu na dhabihu za Wanyama.

**Waebrania 9:13-14** *[13] Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili; [14] basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?*

Tazama maneno haya **KWA ROHO WA MILELE…SADAKA ISIYO NA MAWAA…ITAWASAFISHA DHAMIRA ZENU.** Huu ndio urefu na kimo ambacho dhabihu hii hutenda.

Dhambi huondolewa au husamehewa kwa imani katika dhabihu ya Yesu Kristo. Mungu hana kumbukumbu la dhambi na uovu kwenye Agano la Kristo. Hivyo, mwamini amekamilishwa milele na imefanyika hivyo mara moja.

Msamaha wa dhambi hivyo ni zawadi. Hii haina vigezo na masharti. Msamaha wa dhambi pia sio jambo ambalo Mungu atafanya, ni jambo ambalo Mungu ameshafanya ndani ya Kristo. Mungu haendi kumsamehe mtu kesho au baadae. Kristo – sadaka toshelevu amekwishatolewa, mtu anahitaji kuamini tu na kupokea msamaha wa dhambi.

Zingatia nyakati Paulo anazotumia akizungumzia msamaha wa dhambi kwa waamini hapa;

**Waefeso 4:32** *[32] tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*

MKASAMEHEANE KAMA NA MUNGU KATIKA KRISTO ALIVYOWASAMEHE NINYI.

Tena, **Warumi 4:7** *[7] Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao.*

MAKOSA YAMESAMEHEWA, DHAMBI ZIMESITIRIWA. Heri hapa ni kubarikiwa.

Wamekwishabarikiwa.

**Wakolosai 1:13-14** *[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; [14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;*

MUNGU AMETUOKOA KATIKA NGUVU ZA GIZA…AMETUHAMISHA KUJA KWENYE UFALME WAKE…TUNAO UKOMBOZI NDANI YAKE YAANI MSAMAHA WA DHAMBI.

**Wakolosai 2:13** *[13] Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote;*

AMETUFANYA HAI PAMOJA NAYE, AKIISHA KUTUSAMEHE MAKOSA YOTE.

**Wakolosai 3:13** *[13]mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi.*

BWANA AMETUSAMEHE, VIVYO NASI TUNAWASAMEHE WENGINE.

**1 Yohana 2:12** *[12] Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake.*

ANAWAANDIKIA WAJUE KUWA WAMESAMEHEWA DHAMBI ZAO, KWA AJILI YA JINA LAKE YESU.

Isaya nabii ameweka wazi hili pia…**Isaya 43:25** *[25] Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako.*

MUNGU HUFUTA MAKOSA KWA AJILI YAKE MWENYEWE.

Hivyo, msamaha wa dhambi sio jambo la mtu kuomba asamehewe. Asiyeamini anapaswa kupokea msamaha kwa imani na mwamini anapaswa kuwa na uhakika kuwa amesamehewa; dhambi hazitawekwa juu yake kamwe. Mwamini anao (anamiliki) msamaha wa dhambi. Uzuri zaidi ni kwamba; waamini hatujasamehewa tu dhambi bali pia tumeokolewa katika dhamira ya kujiona wenye dhambi kila wakati. Dhabihu za Wanyama ziliwafanya waendelee kujiona wenye dhambi lakini dhabihu ya Yesu imetuweka huru na dhambi na dhamira ya dhambi. HALELUYA!

**Kwa hiyo, MWAMINI ANAO MSAMAHA WA DHAMBI KWA NJIA YA IMANI NA SIYO KWA SABABU AMEOMBA AU AMESAMEHE WATU WENGINE BALI AMEAMINI DHABIHU YA YESU KRISTO.**

LAKINI **YESU ALIMAANISHA NINI?** Hapa kwenye **Mathayo 6:14** *[14] Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. [15] Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.*

# SURA YA 3

## *KWA HIYO YESU ALIMAANISHA NINI?*

Katika Injili nne, kuna mistari kadhaa yanayoonyesha kuwa Mungu anatusamehe kadri tunavyowasamehe watu wengine. Angalia mistari ifuatayo.

**Mathayo 6:12** *[12] Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.* Pamoja na **Mathayo 6:14-15** *[14] Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. [15] Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.*

Pia, **Luka 11:4** *[4] Utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye. Na usitutie majaribuni [lakini tuokoe na yule mwovu]*.

Ukisoma mistari hiyo, mambo kadhaa, hukujia kichwani kwamba, inaonekana:-

1. Msamaha wa Mungu unategemea namna tunavyowasamehe wengine.

2. Tukishindwa kusamehe basi Mungu naye hatatusamehe. Kwa hiyo sisi ndiyo tunaoamua kama tutasamehewa kwa kusamehe na kutosamehewa kwa kutosamehe.
3. Kiwango au kipimo chako cha kusamehe wengine ni kiwango hicho hicho Mungu atatumia kutusamehe.
4. Msamaha wa Mungu siyo zao la Imani katika Kristo tena bali jitihada zetu za kusamehe. Inageuka kuwa ni kwa matendo.
5. Hii inaondoa sababu ya Yesu kufa na kufufuka. Inaifanya kazi yake kuwa bure na msalaba ubatili mtupu.

**MAMBO YA MSINGI YA KUKUMBUKA KILA MARA UNAPOSOMA VITABU VINNE VYA INJILI**

Vinaitwa ushahidi wa macho (eye-witness account). Ni mambo ambayo watu waliyaona na kuyashuhudia. Kwa hiyo, ni vyema kujua kuwa:-

*1.* Wewe siyo hadhira yao (primary audience). Ijapokuwa vitakufaa wewe leo, lakini mwandishi alikuwa anaongea na watu anaowafahamu yaani Wayahudi amabao ni wanafunzi wa Yesu, waandishi/wazee, mafarisayo, masadukayo, au wengine kama vile Theofilo. Hadhira huamua aina ya lugha na uchaguzi wa maneno na hata mifano. Angalia **Mathayo 13:3** *[3]Akawaambia mambo*

*mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda.*

**Mathayo 13:3,13**

*[3] Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. [13] Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.*

**Mathayo 13:3,34-35**

*[3]Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. [34]Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; [35] ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali.*

**Mathayo 13:53**

*[53] Ikawa Yesu alipoimaliza mifano hiyo, alitoka akaenda zake. Kukataliwa kwa Yesu katika Nazareti*

**Mathayo 21:45**

[45] *Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao.*

**Marko 3:23** *[23] Akawaita, akawaambia kwa mifano, Awezaje Shetani kumtoa Shetani?*

**Mark 4:2,10** ***[****2] Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, akawaambia katika mafundisho yake, [10] Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano.*

**Marko 4:11-13** [11] *Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, [12] ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; Wasije wakaongoka, na kusamehewa. [13] Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?*

**Marko 4:33** *[33] Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia.*

**Marko 12:1** [1] *Akaanza kusema nao kwa mifano; Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akazungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri.*

**Luka 8:10** *[10] Akasema, Ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme wa Mungu; bali wengine kwa mifano, ili wakiona wasione, na wakisikia wasielewe.*

2. Sehemu kubwa ya vitabu hivyo ni ahadi-zinatimia katika ufufuo wa Yesu Kristo. Chapter za mwisho zinaonyesha hayo;

**Luka 24:44** *[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote*

*niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

Angalia Kleopa namwenzake walivyotafsiri kufa na kufufuka kwake. **Luka 24:13-32** *[13] Na tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili. [14]Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia. [15] Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao. [16] Macho yao yakafumbwa wasimtambue. [17] Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea? Wakasimama wamekunja nyuso zao. [18] Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi? [19] Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote; [20] tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha. [21] Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo; [22] tena, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema, [23] wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema kwamba yu hai. [24]*

*Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona. [25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! [26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? [27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.[28] Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. [29] Wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao. [30] Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. [31] Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao. [32] Wakaambiana, Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?*

3. Ufunuo haukuandikwa kwenye vitabu hivyo vinne i.e Inaonekana na kusikitisha kwa Yesu anateswa, kufa na hatimaye kufufuka.

Kama anateswa mwenyewe-

Ufunuo kwenye nyaraka ni kwamba- TULISURUBIWA pamoja naye, TUKAFA pamoja naye, Tukazikwa pamoja naye na Tukafufuka pamoja naye.

**Waefeso 2:4-6** *[4] Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; [5] hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. [6] Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;*

**Wakolosai 2:20** *[20] Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani*

**Warumi 6:8** *[8] Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye.*

**Wagalatia 2:20** *[20] Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*

**Wakolosai 3:1,*3*** *[1] Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. [3] Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.*

Kwenye vitabu vine vya injili inaonekana anateswa mwenyewe, anasulubiwa mwenyewe, anakufa mwenyewe, anazikwa mwenyewe,anafufuka mwenyewe.

Kwahiyo tunatumia nyaraka kupima fundisho kwenye vitabu vine vya injili- PIA nyaraka ziliandikwa “primarily” kwa ajili ya KANISA-WAAMINI tofauti na vitabu vinne(Mathayo-Yohana).

TURUDI KWENYE Mathayo 6:12

Ukakasi upo kwenye mstari wa 12,14 na 15.

Lakini hili tatizo au changamoto ipo Mathayo 6:12-15 tu,angalia pia “Sala ya Bwana” **Luka 11:1-4** *[1] Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake. [2] Akawaambia, Msalipo, semeni, Baba [yetu uliye mbinguni], Jina lako litakaswe, Ufalme wako uje, [Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.] [3] Utupe siku kwa siku riziki yetu. [4]Utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye. Na usitutie majaribuni [lakini tuokoe na yule mwovu].*

**Marko 11:25-26** *[25] Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. [26] Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.*

Unaonekana hapa kote kuwa Msamaha wa Mungu ni wa VIGEZO; Je, ni kweli?

## 4. ANGALIZO

a) Machaguzi ya maneno ya watafsiri yanaweza kuleta uelewa usio sawa- unapotafsiri lugha kwenda lugha nyingine- CHOICE OF WORDS By translators.

Kwanini uchukue “WHAT” ukaacha “WHO” wakati neno moja la kigiriki na “WHICH” **TIS**. Kwa mfano. **Mathayo 5:45/46** [45] *ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.*

b) Watafsiri (Translators) wengi wa Mwanzo walikuwa wakifanya kazi zao za kawaida- wengine hata hawakuwa wakristo-wanaweza wasijue neno gani linaleta maana hasa kulingana na IMANI ya Kikristo.
c) Nyaraka zinaonyesha kuwa Mungu hatoi msamaha kwa kigezo kwamba tunawasamehe wengine kwanza.

Tunatakiwa tumwige Mungu. Angalia **Waefeso 5:1-2** **Waefeso 5:1-2** Hivyo mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa; 2 mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato.

Maneno *Hivyo mfuateni Mungu* yametumika KJV kama **Be ye therefore followers of God** ikiwa ni sawa na kusema be IMMITATORS OF GOD. Ni kitenda cha kumwiga Mungu au kufuata namna Mungu anavyofanya.

Tunaiga nini? Rudi **Waefeso 4:32** *[32] tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*

Inaonekana wazi kuwa siyo sisi tunaosamehe ILI atusamehe ILA tunasamehe kwa kuwa Yeye ameshatusamehe katika Kristo. *We don't inspire God to forgive us, He inspires us to FORGIVE.* Hatumhamasishi Mungu kutusamehe ila yeye hutuhamasisha kusamehe wengine KWA NAMNA alivyotusamehe.

Angalia **Warumi 5:8** *[8] Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. -Alianza yeye.*

d) Kama ingekuwa tunasamehe wengine basi Mungu angesubiri tukomae KIROHO kisha tuwasamehe wengine kisha ATUSAMEHE.

WOKOVU ungekuwa ni jambo sawa na **haliwezekani**.

e) Mungu anasamehe kwanza bure/SANA kisha msamaha huo unazaa upendo na uwezo wa kusamehe wengine

Angalia **1Yohana 3:16-17** *[16] Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.[17] Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?*

Angalia pia alivyoandika kwenye **Yohana 3:16** *[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Huyu ni Mungu amefanya kabla watu hawajamwamini. Alimtoa mwanaye kwanza.

Angalia pia **1Yohana 4:9-11,18-19** *[9] Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. [10] Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. [11] Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana.*

*[18] Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. [19] Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.*

Angalia matumizi ya maneno… *si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi.. ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana… Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.*

Ndiyo maana ya kusamehe (kupenda) kama Yeye alivyotusamehe (alivyotupenda) sisi kwanza.. **Waefeso 4:32** *[32] tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye*

*huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*

Angalia pia na **Wakolosai 3:13 [13]** *mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi.*

f) Yesu (Mungu katika mwili) kwenye vitabu vinne vua injili alisamehe bure au

(a)Hakuwahi kumsamehe mtu baada ya mtu huyo kumsamehe mwingine.

(b) Hakuwahi kumsamehe mtu baada ya KUOMBWA MSAMAHA.

Kwanini tunamwangalia Yesu?

**Yohana 1:18** *Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua*.

Angalia na **Yohana 1:1** *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*

Unganisha na **Yohana 1:14** *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*

Neno= Mungu=Yesu.

Biblia ya TKU (Tafsiri ya Kusoma kwa Urahisi) **Yohana 1:18** *Hakuna aliyewahi kumwona Mungu isipokuwa Mwana peke yake, ambaye yeye mwenyewe ni Mungu, ametuonesha jinsi Mungu alivyo. Yuko karibu sana na Baba kiasi kwamba tunapomwona, tumemwona Mungu.*

Na **Yohana 1:14 TKU** *Neno akafanyika kuwa mwanadamu na akaishi pamoja nasi. Tuliouna ukuu wa uungu wake; utukufu alionao Mwana pekee wa Baba*.

Angalia na **Waebrania 1:1-3** *[1]Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, [2] mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. [3] Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;* | **Wakolosai 1:19** *Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;*

Akarudia **Wakolosai 2:9** *Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.*

Katika mistari hiyo miwili, **yeye** ni Yesu Kristo.

Kwanini tumemwangalia Yesu? Kwa sababu ni Mungu na hana kigeugeu. Angalia **Waebrania 13:8** *Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.*

Sasa Yesu Kristo alisamehe vipi?

Tuanze na **Marko 2:5-10** [5] *Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako. [6] Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao, [7] Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu? [8] Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? [9] Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? [10] Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza).*

Huyu ndugu hakuomba msamaha wowote wala hakusamehe mtu mwingine… ila Yesu ameonyesha kuwa *anayo amri duniani ya kusamehe dhambi.*

Imerudiwa **Luka 5:20** *Naye alipoiona imani yao, alimwambia, Ee rafiki, umesamehewa dhambi zako.*

**Mathayo 9:1-8** [1] *Akapanda chomboni, akavuka, akafika mjini kwao. [2] Na tazama, wakamletea mtu mwenye kupooza, amelala kitandani; naye Yesu, alipoiona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza, Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako. [3] Na tazama, baadhi ya waandishi wakasema nafsini mwao, Huyu anakufuru. [4] Naye Yesu, hali akijua mawazo yao, akasema, Mbona mnawaza maovu mioyoni*

*mwenu? [5] Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? [6] Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (amwambia yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako. [7] Akaondoka, akaenda zake nyumbani kwake. [8] Makutano walipomwona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii*.

Hapa pia alitoa msamaha kama kazi na amri yake au jambo lililoko kwenye mamlaka yake.

Angalia alivyosema, *Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako… 6 Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi*. Watu wakafanya nini? *wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii*.

Angalia pia **Luka 7:36-50** *[36] Mtu mmoja katika Mafarisayo alimwalika ale chakula kwake; akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani. [37] Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya marimari yenye marhamu. [38] Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu-busu miguu yake na kuipaka yale marhamu. [39] Basi, yule Farisayo aliyemwalika*

*alipoona vile, alisema moyoni mwake, Mtu huyu kama angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, naye ni wa namna gani, ya kwamba ni mwenye dhambi. [40] Yesu akajibu akamwambia, Simoni, nina neno nitakalo kukuambia. Akasema, Mwalimu, nena. [41] Akasema, Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili; mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini. [42] Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili. Katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi? [43] Simoni akajibu akasema, Nadhani ni yule ambaye alimsamehe nyingi. Akamwambia, Umeamua haki. [44] Akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simoni, Wamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu; bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. [45] Wewe hukunibusu; lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu yangu. [46] Hukunipaka kichwa changu mafuta; bali huyu amenipaka miguu yangu marhamu. [47] Kwa ajili ya hayo nakuambia, Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana; lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo. [48] Kisha alimwambia mwanamke, Umesamehewa dhambi zako. [49] Ndipo wale walioketi chakulani pamoja naye walianza kusema mioyoni mwao, Ni nani huyu hata asamehe dhambi? [50] Akamwambia yule mwanamke, Imani yako imekuokoa, enenda zako kwa amani.*

Angalia alichosema *Akamwambia yule mwanamke, Imani yako imekuokoa, enenda zako kwa amani.* Mwanamke hakufungua mdomo.. ila Yesu anasema imani yake (kwa Yesu mwenye amri ya kusamehe dhambi) imemwokoa (imempa msamaha wa dhambi kutoka kwa Yesu Kristo).

**Yohana 8:1-11** *[1] [Walikwenda kila mtu nyumbani kwake; naye Yesu akaenda mpaka mlima wa Mizeituni. [2] Hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. [3] Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. [4] Wakamwambia, Mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. [5] Basi katika torati, Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake namna hii; nawe wasemaje? [6] Nao wakasema neno hilo wakimjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama, akaandika kwa kidole chake katika nchi. [7] Nao walipozidi kumhoji, alijiinua, akawaambia, Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe. [8] Akainama tena, akaandika kwa kidole chake katika nchi. [9] Nao waliposikia, wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee hata wa mwisho wao; akabaki Yesu peke yake, na yule mwanamke amesimama katikati. [10] Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Je! Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? [11] Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu*

*akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.]*

Unaona hapa? Hata huyu mwanamke aliyefumaniwa hakuomba msamaha. Yesu anamwambia *Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.* Kutomhukumu maana yake ni kutomhesabia hatia, sawa kabisa na kumsamehe bure. Alisema, Yesu naomba unisamehe? La hasha!.

Namna Yesu alivyosamehe inakubaliana kabisa na nyaraka za mitume zilivyozungumza juu ya Msamaha wa Mungu.

Je, nyaraka zinasemaje namna Mungu anavyosamehe?

**Waefeso 1:7** *Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

(Katika yeye/ katika damu yake tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.)

**Wakolosai 1:14** *ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;*

(Katika yeye tunao msamaha wa dhambi)

g) Kama ilitakiwa tusamehe ili Mungu atusamehe BASI kazi ya Msalaba wa Yesu HAINA maana wala Yesu hakutakiwa KUFA sembuse kufufuka.

Warumi 4:25 isingekuwa na maana. Angalia **Warumi 4:25** *ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki.*

Kutolewa pale ni kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Angalia pia **2 Wakorintho 5:21** *Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*

Angalia… *alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu..*

**2 Wakorintho 5:21** isingekuwa na maana…

Wakolosai 1:14|Waefeso 1:7, Waebrania 8:12-13, 1Yohana 2:12, wakolosai 2:13, Matendo ya mitume 13:38-39, Matendo ya mitume 5:3| 26:18 (mistari hii isingekuwa na maana kabisa)

Warumi 4:6-8,25- mstari wa 25 hueleza huo uheri unavyopatikana, nenda hadi 5:1-2-Ni Neema| Waefeso 2:8-10| Ni Neema.

Zaburi 32:1-2 Zaburi 130:3-4 pamoja na Zaburi 103:8-12

**BAADA ya kusema haya yote, Nini kimetokea kwenye Mathayo 6:12,14,15 na Luka 11:4, Marko 11:25-26.**

Tuanzie Mathayo 5:38-48 kwa sababu ni mtiririko wa mahubiri ya mlimani (Sermon in the mount) ambayo yameanzia Mathayo 5:1.

**Mathayo 5:38-48** *Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino; 39 Lakini mimi nawaambia,*

*Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. 40 Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. 41 Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili. 42 Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo. 43 Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; 44 lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, 45 ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. 46 Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? 47 Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo? 48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*

Yesu anawaonyesha wanafunzi wake kutofanya mambo kama watu wengine, kulipa baya kwa baya au jema kwa jema bali wamwige Mungu (*mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu*) ambaye huwatendea mema watu wote bila kujali hali zao.

Mstari wa 45- unafanana na Waefeso 5:1, *ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni.*

-Huwaangazia jua lake  waovu na wema- bila vigezo, na masharti. Ni Upendo tu kutoka kwake siyo kwa anayeomba.

-Huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki- bila vigezo, na masharti.

Mstari wa 48- Mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu au MTAMWIGA BABA YENU.

Mstari wa 45 na 48- kwa uwazi kabisa, Mungu anasamehe watu wote- Msamaha upo kwake

**Zaburi 130:3-4** *Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? 4 Lakini kwako kuna msamaha, Ili Wewe uogopwe.*

**Hebu sasa tuangalie Sala ya Baba yetu.**

Angalia Mathayo 6:9-15 halafu tuiangalie hatua kwa hatua.

**Mathayo 6:9-15** *Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, 10 Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. 11 Utupe leo riziki yetu. 12 Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. 13 Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele.*

*Amina.] 14 Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. 15 Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu*.

Tuanze na mstari wa 6 *Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje*

Kwa kusema "…*Baba yetu uliye mbinguni*…", Yesu alikuwa akitabiri kuhusu jambo la wakati ujao kwa sababu Mungu hakuwa Baba yao wakati huu kwa vile walikuwa bado hawajazaliwa mara ya pili.

Katika mstari wa 10, anafundisha juu ya Mungu katikati ya wanadamu ambapo ni Neno kufanyika mwili. Huu ni "ufalme wako uje", ufalme wake ulikuwa umekuja katika Kristo Yesu ambaye atatimiza mpango wa Mungu wa kuishi ndani ya wanadamu.

Kwa hiyo maneno "Jina lako litukuzwe" yanarejelea utimizo wa Yesu katika ufufuo wake. Kwa maneno mengine, ufalme kuja na jina lake kutukuzwa inaongelea kufanyika mwili (incarnation) na ufufuo.

Kutoka Mstari wa 11, kuna kiwakilishi muhimu ambacho ameanza nacho kabla, kinapaswa kuendelea kuwepo. bila kuweka kiwakilishi hiki, kile ambacho Yesu alikuwa akisema hapa kinapotea. Viwakilishi "wako" na "lako" "yako" (KJV = Your, You) ni muhimu sana katika maandishi haya.

Andiko linasema

> *"Baba yetu…, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe..."*

Mpaka hapa, kifungu kimezungumza kuhusu kile ambacho Mungu atafanya au amefanya.

**Mathayo 6:11-12** *[11] Utupe leo riziki yetu, [12] Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.*

Aya hii ilionekana kama ombi lililokuwa likifanywa, wakati ambapo ilipaswa kubaki na kiwakilishi kuongelea kile Mungu anafanya au atafanya kama jinsi alivyoanza hapo kabla.

Kwa hivyo, inapaswa kusomeka:

*"...unatupa leo riziki yetu..."*

Hii ni juu ya Mungu, sio jambo la maombi. Yesu anasema kile Baba anachofanya.

Neno *"leo"* linaongelea tukio au ufikiaji malengo (accomplishment). Hairejelei siku fulani ya juma.

**Luka 4:21** *[21] Akaanza kuwaambia, **leo** andiko hili limetimia masikioni mwenu.*

*"***Leo***"* hapa inahusu ukweli kwamba maandiko yalitimizwa.

Kwa hiyo, Yesu alikuwa akifundisha juu ya siku ya ufalme ambayo ni katika/baada ya ufufuo wake.

Tena, huu mstari wa 11 una neno ambalo halipo katika tafsiri ya SUV, angalia tafsiri ya KJV

*"…Give us this day our daily bread…"*

Neno *"daily"* (kila siku) halipo katika SUV.

Tukirejesha kiwakilishi "you" tunakua na;

*"…you give us this day our daily bread…"*

Kama kusema:

*"…unatupa leo mkate (riziki) wetu wa* ***kila siku****"*

Neno *"kila siku"* lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki *"epiousios"* ambalo lina maana ya kutosha yaani kwa kile kinachotosha au kinachotosheleza. Katika Septuagint, kisawe chake cha Kiebrania kinaonekana katika Mithali 30:8

**Mithali 30:8** *[8] Uniondolee ubatili na uongo; Usinipe umaskini wala utajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu;*

Hii ina maana, "kadiri yangu" au kinachotosheleza inarejelea kile ambacho hakimaliziki. Kwa hiyo, hili haliwezi kuwa ombi la vitu vya kimwili badala yake ni kile ambacho ni cha milele, kile kinachodumu.

"Riziki" (Mkate) pia ni lugha ya picha, kwa hiyo, Yesu alikuwa akifundisha kutoka katika kitabu cha Agano la Kale.

**Kumbukumbu la Torati 8:3** *[3] Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyoijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana.*

Kwa hiyo, riziki (mkate) huo ni mfano wa kile ambacho Mungu alisema atafanya. Yesu pia alitumia neno mkate (chakula) kwa njia ya mfano.

**Yohana 6:32-35, 46-51** *[32] Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, si Musa aliyewapa mkate kutoka mbinguni; bali Baba yangu anawapa ninyi mkate wa kweli kutoka mbinguni. [33] Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima. [34] Wakamwambia, Bwana, tupe mkate huu sikuzote. [35] Yesu akawaambia, Mimi ndimi mkate wa uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kamwe; naye aniaminiye hataona kiu kamwe. [46] Si kwamba mtu amemwona Baba, ila yeye atokaye kwa Mungu; [47] Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye yuna uzima wa milele. Mimi ndimi ule mkate wa uzima. [49] Baba zenu walikula mana kule jangwani, wakafa. 50 Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni, kwamba mtu akile wala asife. [51] Mimi ndimi mkate wenye uzima ulioshuka kutoka mbinguni; mtu akila mkate huu, ataishi milele.*

Mkate huu au chakula hiki sio mali au kitu cha kimwili, ni cha milele na ndio maana katika Mstari wa 12 wa Mathayo 6, alizungumza juu ya msamaha wa Dhambi.

Hiki ni kile Mungu anatoa katika ufufuo wa Yesu, chakula kisichomalizika, cha milele, Roho wake, msamaha wake. Hiki ni kile kinachotosheleza.

Mstari wa 12, **Mathayo 6:12** *[12] Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.*

Kusoma kifungu hiki kama kinavyofafanuliwa katika Toleo SUV la bibilia inaonekana kuwa Mungu anaiga msamaha wetu. Kwamba anasamehe sisi tukisamehe. Ingawa, mapema katika sura ya 5, mazungumzo ya Yesu yalikuwa kwamba sisi ndiyo tunapaswa kuwa kama Baba yetu. Tunajifunza na kuiga kwake.

**Mathayo 5:43-48** *[43] Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako. [44] Lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowadhulumu ninyi; [45] ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. [46] Kwa maana mkiwapenda wale wanaowapenda ninyi, mna thawabu gani? hata watoza ushuru hawafanyi vivyo hivyo? [47] Na mkiwasalimu ndugu zenu peke yao, mnafanya nini zaidi ya wengine? hata watoza ushuru hawafanyi hivyo? [48] Basi ninyi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*

Baada ya kuona andiko lililo hapo juu, tunaweza kuona waziwazi kwamba katika sura inayofuata, hawezi kupingana na yale aliyokuwa ameeleza kuhusu kuwa kama Baba wa mbinguni katika muktadha huo huo.

Vinginevyo, je, ingemaanisha kwamba tusiposamehe na tukifanya dhambi Mungu atafanya dhambi ya kutokusamehe vivyo hivyo? Hilo haliwezekani.

**Mathayo 6:9-10** *[9] Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe. [10] Ufalme wako uje. Mapenzi yako yafanyike duniani kama huko mbinguni.*

Neno "kama" limetafsiriwa kutoka kwa neno la Kiyunani "hos". Neno 'hos' lina vigeu sita (6). Baadhi yake ni:

- Kama (as)
- Kama vile (like as)
- Jinsi gani (How)
- Ili kwamba (So that)

Katika muktadha wa mjadala huu, ni wazi kwamba kigeu kinachofaa zaidi ni neno "**ili**". Licha ya ukweli kwamba Yesu alikuwa amefundisha akisema tumwige Mungu, pia tusisahau kwamba alianza sala akieleza yale ambayo Baba anafanya. Hivyo hata hapa haibadiliki, ni kile Baba anafanya.

Baba anafanya nini?

▪ Anatupa ufalme wake - 'ufalme wake uje'.

▪ Mapenzi yake yanatimizwa duniani.

▪ Anatupa leo riziki (mkate) yetu ya kila siku.

▪ Anatusamehe makosa yetu.

Kwa hivyo, maandishi yanaweza kutengenezwa vizuri kama:

> *"Unatusamehe deni zetu ili nasi tuwasamehe waliotukosea."*

Hii inaelekeza umakini wetu kwa ukweli kwamba tunajifunza tendo letu la msamaha kutoka kwa jinsi Baba anavyosamehe. Kwa hivyo, kifungu cha maneno kinachofaa zaidi ni "ili";

**Mathayo 6:13** *[13] na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu; Amina*.

Kwa kuwa Yesu anatuambia kile Baba anachofanya, hatupaswi kusahau kiwakilishi cha kumhusisha Yeye.

Mstari huo unaweza kueleweka vyema zaidi kama:

> *"haututii majaribuni..."*

Neno "bali" lililotumika hapo lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "alla" ambalo linaweza kumaanisha “yaani” (that is)

Kwa hivyo, kauli inaweza kusomeka namna hii:

> *"Haututii majaribuni, YAANI, unatuokoa na yule mwovu"*

Kwa hiyo, maombi hapa yanahusu ufalme wa Mungu, yaani, katika kile ambacho Mungu anafanya na atakachofanya. Mungu amekuja kati ya wanadamu na mapenzi yake yako duniani. Anatupa mkate wetu wa kila siku yaani anasamehe dhambi, anatuokoa na yule mwovu; huo ni ufalme wa Mungu.

Kuachwa kwa kiwakilishi kumhusisha Mungu katika utendaji inatupa maana nyingine tofauti kabisa.

**Mathayo 6:14-15** *[14] Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. [15] Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu*

Ngoja tuangalie KJV **Matthew 6:*14*** *For if ye forgive men their trespasses, your heavenly Father will also forgive you:*

Tushughulikie Kingereza hapa… neno **<u>their</u>** lina maana kadhaa.

*For if ye forgive men* **<u>their</u>** *trespasses, your heavenly Father will also forgive you:*

Neno "**<u>their</u>**" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**<u>autos</u>**". Lina maana ya kusema kadaha ikiwa na pamoja na "vivyo hivyo"; “njia hiyo hiyo”, “namna hio hio” (same way) au "sawa" (same).

Tutumie same au same way.. ITASOMEKA…

*"For if you forgive men's trespasses, you forgive, **same** as your heavenly father"*

KISWAHILI..

*"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, mwasamehe **sawa** na Baba yenu wa mbinguni"*

Hivyo ndivyo ilivyopasa iwekwe na wafasiri wa Kiswahili.

Hii ni kwa sababu kutokana na andiko hilo, ni wazi kwamba haombi Baba wa mbinguni atuige sisi, bali anawaomba wasikilizaji kuakisi tabia ya Baba wa mbinguni.

**Mathayo 6:15** *[15] Bali msipowasamehe watu makosa yao, **wala Baba yenu hatawasamehe** ninyi makosa yenu*

**Matthew 6:15** *But if ye forgive not men their trespasses, **neither** will your Father forgive your trespasses.*

Shida hapo ni neno **NEITHER** ambalo ni neno la Kigiriki "**oude**". Linamaanisha **NOT AS au NOT AS MUCH.**

Kwenye SUV, Kifungu cha maneno "wala… hata-" kilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**oude**". Inamaanisha **"sio kama"** (not as).

Mstari wa 15, kwa hiyo, unaweza kueleweka vyema kama:

*" Bali msipowasamehe watu makosa yao, **SI KAMA** Baba yenu wa mbinguni awasameheavyo ninyi makosa yenu"*

Kwa maneno mengine, kitendo cha kutosamehe hakitaakisi asili na tabia ya Baba wa mbinguni. Hata hivyo, anasema anafanya mema ili sisi tutende mema.

Yesu, kwa hiyo, anaelekeza umakini wao kwa msamaha unaopatikana kwa Baba na kutangulia kutabiri (prefigure) kitendo cha mwamini cha msamaha kama kielelezo cha msamaha wa Baba.

Kwa hiyo, Yesu alihubiri injili katika kuwafundisha jinsi ya kuomba. Wanapaswa kuthibitisha kile anachotimiza katika ufufuo.

## Kama Mungu ndiye mtendaji ILI SISI TUIGE BASI tungeendelea kusema…..

Your kingdom come

**(Ufalme wako unakuja)**

Your will be done

**(Mapenzi yako yatatimizwa)**

You give us our daily

(Unatupa riziki yetu )

You forgive our debts –

(Unatusamehe deni zetu)

You lead us NOT………. You deliver

(Hautuingizi katika majaribu…. Unatuokoa… )

Yours is the kingdom……..

(Ufalme ni wako)

Hii sala ilitakiwa kuwa hivi-BAADA YA UFUFUO

- Baba yetu uliye Mbinguni- (Hapa ni kutofautisha na Biological)
- Jina lako litukuzwe- (Ufufuo wa Yesu ni utukufu wa Baba)
- Ufalme wako uje/Utakuja- (Kukaliwa na Roho after Resurrection)
- Mapenzi yako yatimizwe ulimwengu (Mapenzi ya Mungu ni kutolewa kwa mwili wa Yesu Kristo kwa ajili ya dhambi zetu)
- Utatupa mkate siku hii- (Kifo na Ufufuo wa Yesu)
- Unatusamehe deni zetu ILI na sisi tuwasamehe wadeni zetu- Tumeona kwenye nyaraka.
    - Hututii majaribuni ILA Unatuokoa na yule mwovu
    - Kwa kuwa ufalme ni wako na nguvu na utukufu hata milele.

(14) kwa maana mkiwasamehe watu makossa yao NI KAMA Baba yenu wa mbinguni anavyowasamehe ninyi

(15) Bali msipowasamehe watu makossa yao SI KAMA Baba yenu anavyowasamehe ninyi makossa yenu.

Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa BIBLIA haifundishi kuwa Mungu anasubiri tusamehe ili atusamehe na tusiposamehe naye pia hawezi kutusamehe. Kwa sababu,

1. Haikubaliani na tabia ya Mungu.
2. Haikubaliana na lengo la kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.
3. Ingepingana moja kwa moja na maelezo yaliyoko kwenye nyaraka.

**Vitabu Vingine Vya Shemeji Melayeki**

**KISWAHILI**

1. *Ukombozi Reloaded*
2. *Kufunga Reloaded*
3. *Moyo wa Baba*
4. *Akaanza Kutoka Musa I*
5. *Yanipasa Nifanye Nini Nipate Kuondoka?*

6. *Uinjilisti na Uanafunzi*
7. *MAOMBI: Bwana Tufundishe Sisi Kusali*
8. *Chapa Ya Kudumu*
9. *Msimzimishe Roho*
10. *Akaanza Kutoka Musa II*
11. *Kwa Kuwa Sasa Nimeokoka!*
12. *UFUATILIAJI: Namna ya kuwafutualia wanafunzi wapya!*
13. *Nataka Kumwona Yesu – Kijitabu cha 1-4 (watoto)*
14. *Niko Tayari kwa Ndoa?*

**ENGLISH**

1. *Evangelism and Discipleship*
2. *Believer's Eternal Seal*
3. *Now, That I am Born Again!*
4. *Seeing Jesus Christ Book 1-4 (Children's Book)*

## KUHUSU SISI

Huduma ya **Global Family Gatherings** imejikita katika kufundisha Neno la Mungu kwa uchambuzi wa Maandiko hatua kwa hatua. Nia yetu hasa ni kuishi katika mpango wa Mungu wa kwenda kuhubiri Injili na kutengeneza wanafunzi. Mwisho wa siku tuhakikisha kila mtu, kila mahali amefikiwa na kuimarisha katika kweli ili awe mtu

imara na mwenye kutimiza mapenzi ya Mungu hapa duniani.

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
Instagram: *apostleshemejimelayeki*
Facebook: *Apostle Shemeji Melayeki*
YouTube: *Apostle Shemeji Melayeki*

Kufika kwenye ibada zetu na kambi za mafundisho ya neno la Mungu tumia simu +255 714 548 565.

Ukitaka kuwa sehemu ya watu wanaowekeza fedha zao katika kutusaidia kufika injili kwa watu wengine kwa njia ya maandishi na redio tumia +255 714 548 565.

Website yetu: http://globalfamilygatherings.co.tz
Telegram: https://t.me/apostleshemeji
Youtube: https://youtube.com/@shemejimelayeki
Whatsapp channel
https://whatsapp.com/channel/0029VaBdRe5LCoX4y2PpaX3u

**Mafundisho kwa njia ya audio**

https://globalfamilygatherings.co.tz/messages/

**Vitabu vyetu nakala tete**

https://globalfamilygatherings.co.tz/our-books/